# Masihi

*L.M. Abdallah*

# YALIYOMO

AMHED NA HAMDI....................1

MWANA KONDOO WA MUNGU....................2

NENO LA MUNGU....................4

DHABIHU YA MUNGU....................6

DHAMBI....................9

MTOTO WA IBRAHIMU....................12

MUNGU NI MMOJA....................15

MUGU NA MWANADAMU....................19

ORODHA YA VIFUNGO VYA BIBLIA....................20

# AHMED NA HAMDI

Ahmed aliajiriwa katika ofisi. Kusema ya kwamba alikuwa na huzuni katikakazi yake hakungekuwa ukweli, ila tu aliipata kuwa ngumu kuendelea mbele na mkuu wa idara, ambaye hakumpatia Ahmed nafasi yoyote kujitambua.

Punde idara ilipoandaliwa mradi mgumu, tajiri wake kawaida alihakikisha kwamba ni yeye pekee ambaye alichukua sifa yote.

Kwa mara nyingi Ahmed alifikiria kubadilisha kazi yake lakini bahati haikumwangukia na ilikuwa vigumu kupata kazi nzuri hata ikwamuda tu. Mbali na hayo, mshahara wake ulikuwa juu kuliko mishahara katika kazi nyingine zilizopatikana. Hii ilimbidi Ahmed kubaki katika shirika lile lile. Pesa zilikuwa tegemeo kuu kwa sababu alizihitaji kwa mke na watoto wake watatu. Ahmed aliona fahari kwa ajili ya watoto wake, hasa yule Hassan, mvulana wake mkuu ambaye alikuwa masomoni katika chuo kikuu cha ufundi.

Siku moja kitu kilitendeka ambacho kilibadilisha kazi yake kuwa bora. Hamdi alijiunga na idara ya Ahmed. Hamdi ambaye alikuwa mdogo kuliko Ahmed, alikuwa mchangamfu na mwenye furaha na ilikuwa rahisi kuendelea naye. Hatimaye Ahmed alikuwa amempata rafiki wa kufanya naye kazi.Walianza kushiriki pamoja katika chakula cha mchana na tena kukutana jioni. Hamdi pia alikuwa ameolewa, na Mungu alikuwa amewabariki kwa kuwapa watoto wanne wazuri, wavulana wawili na wasichana wawili.

Ahmed na Hamdi walikuwa marafiki wakuu na kila mara walitembeleana: kila mmoja kwa nyumba ya mwingine. Walipenda kuketi chini kwa kikombe cha chai na kuzungumza. Masaa yalipita upesi wakizungumza kuhusu cho chote kile. Kwanza walizungumzia kuhusu kazi ofisini, lakini jinsi masaa yalizidi kupita, walijadili juu ya maisha au maswali yahusuyo maisha. Ahmed na Hamdi, wote wawili, walikuwa watawa kamili lakini hawakuwa na imani moja. Ahmed alikuwa mwislamu na rafiki yake mkuu; Hamdi alisoma Biblia kila wakati na alikuwa mfuasi wa Masihi (Al-Masihi).

Kilichomshangaza Ahmed zaidi ni kwamba alipozidi kumfahamu Hamdi pia alizidi kuheshimu imani yake na maisha yake na Mungu wake. Ahmed alifahamu kwamba rafiki yake alifurahia uhusiano mzuri karibu na Mungu, kitu ambacho yeye mwenyewe alikuwa bado kuona na hiki kilimfanya awe na hamu

Zaidi kujua sababu yake. Ahmed akafikiri ya kuwa maisha yake Hamdi pamoja na Mungu wake yalishikana na Masihi. Kwa njia nyingine Ahmed pia alimwamini Masihi, hata ingawa si kwa njia moja. Aliamini yote yaliyoandikwa ndani ya Koran kuhusu Yesu, mtoto wa Mariamu (Asia Abn Mariam), na alikuwa na heshima ya ndani kwa Masihi.
Alijua kwamba Masihi alikuwa amezaliwa na Bikira Mariamu (Mariam Al-Athra), na kwamba alikuwa amefanya ishara nyingi kibali cha Mungu na kwamba alikuwa amepokea injili (Al-Indijl) kutoka kwa Mungu. Lakini piaAhmed alifahamu ya kwamba alijua machache sana kumhusu Masihi, na tamaa yake iliendelea kumshurutisha ili aendelee kutafuta na kujua zaidi kumhusu mtume huyu mkuu (rasol), ambaye alikuwa amepewa majina mengi ndani ya Korani.
Siku moja Ahmed alizidiwa na tamaa nyingi, akaamua kumwuliza rafiki Hamdi kuhusu Masihi. Uthabiti huu ulisababisha mazungumzo mengi ya kuvuta.

## MWANA KONDOO WA MUNGU

"Niambie kuhusu Yesu, mtoto wa Mariamu!" Ahmed alimsihi Hamdi.
"Ningependa kweli kujua sana kumhusu yeye."
Hamdi alifikiri kwa muda mfupi, kisha akasema, "Kama unataka kujua kwa sababu gani Masihi alikuja ulimwenguni, kwanza unahitaji kufahamu kuhusu dhabihu."
"Dhabihu? Inamaanisha nini? akastaajabu Ahmed.
Hamdi aliendelea, "Tunaona maana ya dhabihu kupitia sherehe ya dhabihu (Id Al-Athha). Unajua wakati Mungu alimwambia Ibrahimu (Sayedna Ibrahimu) kumtoa mwanawe kuwa dhabihu. Ni kipi kingalitendeka kwa mtoto wa Ibrahimu kama Mungu (Allah) hangalitoa fidia, (fida) badala yake",

"Isaka angalikufa," Ahmed alisema. "Hiyo ndiyo maana ya dhabihu," Hamdi akajibu. "Mmoja anakufa kwa badala niaba ya mtu mwingine. Mungu alimtuma kondoo dume ambaye alitolewa dhabihu badala ya Isaka. Niko nafasi sawa sawa na kondoo wa Ibrahimu. Niko chini ya nguvu za mauti, "Hamdi akasema." Maneno yako yana maana gani?" Ahmed akauliza huku akistaajabu kidogo.

Hamdi akajibu kwa bidii. "Imeandikwa katika Biblia (Kitabu Kitakatifu).

**MSHAHARA WA DHAMBI NI MAUTI (1)**

"Mshahara wa dhambi zangu ni mauti. Mauti Mimi ni mwenye dhambi. jamani wengine waniona kama mcha Mungu wa kweli; ninamwomba Mungu kila siku, nasoma kitabu chake na kumtumikia. Lakini mbele yake mimi ni mwenye dhambi. Je, kuna mtu mtakatifu ila Mungu?" aliuliza Hamdi.

"La!" akajibu Ahmed.

"Hakuna ila Mungu tu ni mwenye haki. Kwa hiyo mbele yake Mungu sisi sote tu wenye dhambi, sivyo?" Hamdi aliuliza.

"Ndiyo, hiyo ni kweli," Ahmed akakubali.

"Basi, mimi ni sawa na mtoto wa Ibrahimu. Niko chini ya nguvu ya mauti. Lakini wapi dhabihu kwa dhambi zangu?"

"Je, Mungu hajatuma dhabihu kama fidia kwa dhambiu zangu?" akauliza Hamdi. Ahmed hakujua na la kusema. Hamdi akaendelea, "Yohana Mbatizaji (Yahya Abn Zakaria) aliishi wakati mmoja na Masihi. Wakati wa kwanza alipomwona Masihi, alisema:-

**TAZAMA, MWANA-KONDOO WA MUNGU, AICHUKUAYE DHAMBI YA ULIMWENGU! (2)**

Masihi hakuwa mwana kondoo wa mwanadamu. Alikuja kutoka kwa Mungu. Alikuja kutoka juu Roho Mtakatifu wa Mungu (Roh Allah) akamfunikia Bikira Maria (Mariam). Alishika mimba na akamzaa mtoto wa kiume. Kama ujuavyo anaitwa 'Yesu, mtoto wa Mariamu', na 'Neno la Mungu' (kalimat Allah) na 'Roho Mtakatifu wa Mungu' (Roho Allah), Alikuwa Mtakatifu.

Alikuja kutoka mbinguni kama Mwana-kondoo wa Mungu, Masihi alithibitisha kwamba alikuwa Mwana-kondoo wa Mungu kwa kuishi maisha matakatifu mbele ya Mungu. Hakuna wakati hata mmoja alipotakiwa kusema ,"Nimemwomba Mungu msamaha wa dhambi (Astaghfer Allah Al-Azim), kwa sababu alikuwa mkamilifu Mwana-kondoo wa Mungu. Lakini kwa sababu alikuja kama Mwana-kondoo wa Mungu kuchukua dhambi ya ulimwengu, ilimbidi awe dhabihu. Hii ilitendeka alipojitoa kwa mapenzi yake, akafa Akafufuka kutoka wafu, akapaa mbinguni. Na siku moja atarudi duniani."

Hamdi alinyamaza kwa muda mfupi, huku akimtazama Ahmed, akaendalea, "Nimo katika nafasi moja sawa na mtoto wa Ibrahimu. Niko chini ya nguvu ya mauti. Lakini kuna dhabihu kwa ajili ya dhambi zangu kupitia kwa Masihi, Mwana-kondoo mtakatifu wa Mungu. Sasa, kupitia kwa Mwana-kondoo huyo, Mungu hutoa msamaha wa dhambi zetu zote, na uzima wa milele Paradisoni.

(djanna). Masihi alizichukua dhambi zote za wanadamu pamoja na zako, Ahmed." Ahmed aliketi kimya kwa muda mrefu akifikiri. Nipo akasema, "Ikiwa Masihi alichukua dhambi zote za ulimwengu, hakuna haja nife ... Hivyo tayari nimepokea uzima wa milele."

"Ahmed," akaendelea Hamdi, "Tuseme ya kwamba ni siku yako ya kuzaliwa na Masihi akija na zawadi na agonge mlangoni mwako. Aseme kwako, Ahmed, ningependa kukupatia zawadi ya msamaha kwa dhambi zako zote, uzima wa milele na maisha mapya pamoja na Mungu tangu leo hii. Lakini kuna masharti. Lazima utubu na uungame dhambi zako na kupokea msamaha kupitia dhabihu yangu. Ukiipokea zawadi hiyo ni yako bila shaka. Usipoipokea si yako". Ahmed aliketi akiwaza. Alijisikia mpotevu na hakuwa na la kusema. "Labda unafikiri kwamba huo ulikuwa mfano wa hali ya kigeni sana," alisema Hamdi, "lakini kila mara mtumishi wa Bwana anaeleza njia ya Mungu kupitia kwa Masihi, ni kama Yesu, mtoto wa Mariamu alishiye na aliyefufuka, anagonga katika mlango wetu. Anasema katika Biblia:-

**TAZAMA, NASIMAMA MLANGONI, NABISHA; MTU AKIISIKIA SAUTI YANGU, NA KUUFUNGUA MLANGO, NITAINGIA KWAKE, NAMI NITAKULA PAMOJA NAYE, NA YEYE PAMOJA NAMI. (3)**

Hamdi akaongeza, "Kufungua mlango wangu kwa Masihi na kumwalika kwa maisha yangu, tule pamoja mkate wangu na kuishi pamoja, ni sawa na kupokea zawadi ya Mungu iliyotolewa kwangu na kwa awaye ye yote".

"Ninataka ujue, Hamdi, kwamba kile umeniambia kuhusu Masihi kimenigusa sana. Nitahitaji muda zaidi kwa mazungumzo yetu. Lakini nataka kusikia zaidi kuhusu Masihi tutakapokutana wakati ujao."

> "Al-salamo aleikum" - "Amani na ikae ndani yenu."
> "Aleikum al-salam" - "Na ikae ndani yenu pia".

## NENO LA MUNGU

"Ulichoniambia wakati uliopita kuhusu Yesu, mtoto wa Mariamu, kilinipa mawazo mengi sana". alianza Ahmed kwa hadhari. "Usijisikie vibaya lakini nina maswali mengi ningependa kupata majibu yako kabla ya kuendelea na mazungumzo yetu kuhusu Masihi".

"Naam, endelea!" Hamdi akajibu akifikiri alifahamu yale Ahmed alitaka

kusema. “Basi, Hamdi akaendlea kwa hadhari. “Unajua sisi Waislamu hutegemea viatbu vya mbinguni, Al-Tawrah (vitabu vitano vya Musa), Al-Zabor (Zaburi), Al-Indjil (Injili takatifu ya Yesu) na Korani. Lakini nimefunzwa kwamba vitabu hivyo vyote. isipokuwa Korani, vimegeuzwa na Wayahudi na Wakristo kuwa vitabu vya uwongo na kwa hivyo hatuwezi kuamini yale yaliyoandikwa ndani yao. Biblia ile takatifu unayoiamini ni ya kudanganya (moharraf) kwa kuchanganyika ukweli na uwongo”.

“Unaweza kutoa ushahidi wa historia kuthibitisha maoni hayo yako?” akauliza Hamdi.

Ahmed alifikiria kidogo na kushtuka kwamba alikuwa hajasikia chochote isipokuwa maneno yasio na msingi.

Hamdi akaendelea, “Unaweza kuniambia ni lini danganyo hilo la uongo lilifanyika au jinsi ilivyowezekana kupokelewa?”

“La. siwezi”. Ahmed akasema., akiwa na wasiwasi kidogo. “hakuna hata mmoja ambaye amenipa majibu kwa maswali kama hayo”.

Baada ya muda kidogo Hamdi akauliza, “Unafikiri ingewezekana kugeuza maana ya Korani?”

“Astaghfer Allah!” (Ninaomba Mungu msamaha!) kalia Ahmed. “Hiyo haingewezekana kabisa. Waamini hawangemruhusu mtu ye yote hata kuigusa Korani”.

Hamdi akajibu, “Kwa nini unafikiri tunaiangalia Biblia kuwa tofauti?

Unafikiri waamini wa kweli wangemruhusu mtu mwingine kubadilisha maandiko matakatifu na badala yake kuleta Biblia potovu? Naamini katika Mungu muumba mbingu na nchi, Mungu ayajuaye yote, aliye juu zaidi ya wote.

Yeye aliyempa mwanadamu neno lake, pia ana nguvu kulihifadhi neno lake lisipotoshwe.

Akimkodolea Ahmed macho, Hamdi akauliza, “Ahmed, unaamini kwamba chochote kinachotendeka kinalingana na mapenzi ya Mungu?”

“Ndiyo, naamini hayo, “akajibu Ahmed.

Hamdi akaendelea, “Je! unaamini kweli kwamba Mungu angetoa neno lake kwanza kwa ulimwengu na kisha aamue liwe potovu? Au Mwenyezi Mungu hana uwezo kuhifadhi neno lake lisipotoshwe?”

“Kwa kweli, Mungu ana uwezo kulinda neno lake lisipotoke”. akakubali Ahmed.

“Je! unajua, Ahmed, kwamba Biblia ni kitabu cha ajabu?Kiliandikwa yapata miaka 1400. Kina vitabu vitano vya Musa (Al-Tawrah), Zaburi (Al-Zabor), IInjili (Al-Indjilo), na vitabu vingine vilivoandikwa na watumwa wa Mungu (rasol),

na manabii (anbia). Biblia imegawanyika katika sehemu mbili: Agano la Kale - sehemu ambayo inakuhusu wakati kabla ya kuzaliwa kwake Masihi, na Agano Jipya - inayokuhusu wakati baada ya kuzaliwa kwake Masihi katika ulimwengu Biblia iliandikwa katika lugha tatu mbali mbali".
"Ni lugha zipi hizo?" akashangaa Ahmed.
"Ilianmdikwa katika Kiebrania, Kiaramaiki na kiyunani", akajibu Hamdi. Mungu aliwatumia watu mbalimbali alipotupa sisi neno lake. Wengine walikuwa wafalme au wakuu wa serikali. Wengine walikuwa wachungaji au wavuvi. Biblia ni mwujiza kutoka kwa Mungu, kwa sababu hata ingawa wakati ilipoandikwa ulikuwa mrefu na watu walioiandika walikuwa wengi, Biblia inajumlisha yote. Kuna lengo moja katika Biblia nzima, ni lengo hilo, Ahmed - Masihi (Al-Masihi)".

"Ni kweli kwamba Mungu alizungumzia juu ya Masihi kwa miaka 1400?" Ahmed akasema kwa mshangao.
"Ahmed," akasema Hamdi akiwa mchangamfu, "Mungu amezungumza juu ya Masihi tangu mwanzo hadi leo hii".
"Inawezekana hivyo kweli?" Ahmed akasema mwenye wasiwasi.
"Ndiyo, inawezekana, kwa sababu kila kitu mbele yake Mungu kinawezekana". Hamdi akijibu. "Lakini tunaweza kujadiliana kuhusu hayo tukutanapo wakati mwingine ujao".
"Ninatazamia hayo sana," alisema Ahmed.

"Al-salamo aleikum"
"Aleikum al-salam".

**DHABIHU YA MUNGU**

"Nina hamu kujua jinsi gani Masihi alivyokuwa lengo kuu katika Biblia nzima". Ahmed alisema
"Je! unakumbuka wakati tulipozungumza juu ya Masihi kama Mwana-kondoo wa Mungu aliyechukua dhambi zetu? akauliza Hamdi.
"Ndiyo." akajibu Ahmed, ningeyasahauje?"
Mungu alikuwa akimfundisha mwanadamu kuhusu dhabihu katika historia nzima hadi wakati wa Yesu, mtoto wa Mariamu," Hamdi akasema.
"Kwa njia gani?" akauliza Ahmed.
"Ni watu wangapi walikuwepo wakati wa Kaini (Qabil) na Habili

(Habil)?" Hamdi akauliza. Ahmed akafikiri kidogo, kisha akajibu. "Wanne - Adamu, Hawa, Kaini na Habili".
"Watu wanne tu," akasema Hamdi, "na walifahamu ya kuwa iliwapasa kumwabudu Mungu kwa kutoa dhabihu; walijuaje hayo?" Hamdi akauliza na kuendelea, "Kwa sababu Mungu yu mtakatifu, lakini mwanadamu ni mwenye dhambi na anahitaji fidia kwa dhambi zake. Nuhu (Saydna Noh) alimwabudu Mungu kwa dhabihu. Ibrahimu (Saydna Ibrahim) alimwabudu Mungu kwa dhabihu kwa dhabihu. Musa (Sayedna Musa) alimwabudu Mungu kwa dhabihu. Daudi (Sayedna Dawoud) na mitume wote na manabii walimwabudu Mungu kwa dhabihu". Hamdi akaongeza, "Na mimi ninamwabudu Mungu sawa na mitume na manabii".
"Laa, sasa unafanya mzaha, Huendi sokoni kununua kondoo kumtolea Mungu dhabihu". alisema Ahmed, huku akikunjua uso wake kwa furaha. "Namwabudu Mungu kupitia Masihi, Mwana-kondoo wa Mungu, aliyejitwika dhambi zangu wakati alipotolewa kuwa dhabihu". Hamdi akaendelea. "Imeandikwa katika Biblia takatifu.

**KWA SABABU MUNGU NI MMOJA, NA MPATANISHI KATI YA MUNGU NA MWANADAMU NI MMOJA, MWANADAMU KRISTO YESU: AMBAYE ALIJITOA MWENYEWE KUWA UKOMBOZI KWA AJILI YA WOTE (1)**

"Mungu ni mmoja tu, na mpatanishi kati ya Mungu na sisi ni mmoja, Masihi, aliyetoa nafsi yake kama fidia kwa wote, yaani kwa wewe pia, Ahmed. Katika historia nzima hadi leo hii, watu wamemwabudu Mungu aliye hai kwa dhabihu".
"Nafikiri nimeanza kufahamu kile unachotaka kuonyesha. Lakini inakubidi ueleze kidogo zaidi ili nipate kufahamu picha nzima". Ahmed aliyekuwa na mawazo mengi akasema.
Kitambo kidogo baadaye, Hamdi alijibu, "Mungu alifichua maana sababu ya dhabihu katika historia hasa kupitia Musa katika vitabu vyake vitano. Jumla ya mafundisho ya torati (Al-Sharia) kuhusu dhabihu kama fidia kwa dhambi ni wazi kutoka kwa maandiko haya:-

**NA KATIKA TORATI KARIBU VITU VYOTE HUSAFISHWA KWA DAMU , NA PASIPO KUMWAGA DAMU HAKUNA ONDOLEO. (2)**

"Lakini je! mafundisho hayo yote kuhusu dhabihu, yana uhusiano gani na Yesu, mtoto wa Mariamu?" Ahmed akauliza. "Basi". Hamdi akajibu. "mafundisho kuhusu maana ya dhabihu ni sawa na nabii nyingi kuhusu Masihi. Miongoni mwa manabii hao ni ubashiri kwamba wakati Masihi atakapokuja duniani, angekuwa dhabihu kama fidia kwa dhambi zetu.

Hamdi alichukua Biblia mkononi na akaifungua. Akamwonyesha Ahmed sehemu fulani akisema, "Jionee mwenyewe maelezo halisi kuhusu dhabihu ya Masihi kama nabii Isaya alivyoiandika miaka 700 kabala ya kuja kwake Yesu:-

**HAKIKA AMEYACHUKUA MASIKILITKO ETU, AMEJITWIKA HUZUNI ZETU; LAKINI TULIMSHANIA YA KUWA AMEPIGWA, AMEPIGWA NA MUNGU, NA KUTESWA. BALI ALIJERUHIWA KWA MAKOSA YETU, ALICHUBULIWA KWA MAOVU YETU; ADHABU YA AMANI YETU ILIKUWA JUU YAKE, NA KWA KUPIGWA KWAKE SISI TUMEPONA. SISI SOTE KAMA KONDOO TUMEPOTEA; KILA MMOJA WETU AMEGEUKIA NJIA YAKE MWENYEWE; NA BWANA AMEWEKA JUU YAKE MAOVU YETU SISI SOTE. ALIONEWA, LAKINI ALINYENYEKEA, WALA HAKUFUNUA KINYWA VILE KONDOO ANYAMAZAVYO MBELE YAO WAKATAO MANYOYA YAKE; NAAM, HAKUFUNUA KINYWA CHAKE. (3)**

Ahmed, akiguswa sana na maneno ya unabii, akasema na ungao, "Unasema kwamba hayo yaliandikwa miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwake Yesu, mtoto wa Mariamu?"
"Ndiyo," Hamdi akasema. "Kulingana na manabii, Masihi angeshuka kutoka jamii au ukoo wa Daudi. Daudi, aliyeishi miaka elfu moja kabla ya Masihi, anatoa maelezo kamili na sahihi kumhusu mtoto wake wa kiume, aliyekuwa aje, halafu asulubiwe. Kusulibiwa kulikuwa kifo kirefu na chenye uchungu mwingi. Punde si punde mifupa ya aliyesulibiwa iliteguka na licha ya hayo, na pia aliteseka na kiu kikali. Nabii Daudi anasema katika maandiko:-

**NIMEMWAGIKA KAMA MAJI, MIFUPA YANGU YOTE IMETEGUKA, MOYO WANGU UMEKUWA KAMA NTA, KUYEYUKA NDANI YA MTIMA WANGU. NGUVU ZANGU ZIMEKAUKA KAMA GAE, ULIMI WANGU WAAMBATANA NA TAYA ZANGU: UNANIWEKA KATIKA MAVUMBI YA MAUTI KWA MAANA MBWA WA MENIZUNGUKA; KUSANYIKO LA WAOVU WAMENISONGA; WAMENIZUIA MIKONO NA MIGUU. NAWEZA KUHESABU MIFUPA YANGU YOTE; WAO WANANITAZAMA NA KUNIKODOLEA MACHO. WANAGAWANYA NGUO ZANGU, NA VAZI LANGU WANALIPIGIA KURA (4)**

"Daudi aliandika haya hata wakati wake kusulibiwa hakujatumika kama njia ya kufisha. Njia hii ilianza kutumika baadaye, na ilitumiwa na Warumi wakati wa Masihi".
"Kwa hiyo unataka kusema kwamba utabiri huo umetimizwa wakati wa Yesu, Mwana wa Mariam?" Ahmed akauliza. "Ndivyo, tena si hayo tu, lakini nabii nyingi zimetimizwa halisi kupitia Masihi". akajibu Hadi. "Masihi mwenyewe alithibitisha mara nyingi kwamba alikuja kutoa nafsi yake na uhai wake kama fidia (fida) Alisema juu yake:-

**KWA MAANA MWANA WA ADAMU NAYE HAKUJA KUTUMIKIWA, BALI KUTUMIKA, NA KUTOA NAFSI YAKE IWE FIDIA YAWENGI (5)**

"Ahmed, Je? umefahamu sasa jinsi mafundisho ya Mungu kuhusu dhabihu kwa dhambi za mwanadamu yamedhihirisha katika Biblia nzima na jinsiyametimizwa kupitia Masihi?"
"Hamdi", Ahmed akasema, "sijawai kusikia hayo. Ni mambo ya kupdneza sana. Ninataka muda zaidi kufukuru. Lakini usiwe na mashaka, nitarudi hivi karibuni na maswali zaidi".
"Tafadhali, pokea Biblia hii kama zawadi kutoka kwangu!" Hamdi akasema. "Anza kusoma Agano Jipya, sehemu ambayo inasema kuhusu Masihi na maisha yake, na miujiza na mafundisho yake ya ajabu!"
"Asante!" Ahmed akasema, "Nimesikia mengi kuhusu 'watu wa vitabu' (ahl-al-kitab), lakini sijawai kusoma kitabu chenyewe. Ninatazamia mbele kwa furaha kusoma zaidi kuhusu miujiza (Ishara) na mafundisho yake Yesu, mwana wa Mariamu"

"Al-salamo aleikum"
"Aleikum al-salam"

## DHAMBI

"Hamdi", Ahmed alianza kwa upole, "tangu tulipokutana wakati uliopita, nimekuwa nikifikiria juu ya Masihi na jinsi alivyotoa nafsi yake kama fidia kwa dhambi za wanadamu. Lakini kuna jambo moja ninahitaji kujua. Dhambi (al-khati ya) inatoka wapi, na ni vipi kila mwanadamu anapata shida kutokana na dhambi? Unaweza kuyaeleza hayo?" Ahmed aliuliza kwa sauti nzito. "Ndiyo, nadhani nitaweza kuyaeleza, "Hmdi akajibu kwa kufikiri sana. "Lakini ingefaa turudi nyuma hadi mwanzo tujue chanzo cha dhambi. Kaatika kitabu cha torati, yaani vitabu vitano vya Munga, tunasoma kwamba baada ya kuumba ulimwengu nabinadamu Mungu alimweka mwanadamu katika Paradiso (djanna). Pale Paradiso, mwanadamu alikuwa mtakatifu na aliishi maisha matakatifu na ya kamilifu pamoja na Mungu. Lakini jinsi ujuavyo, kitu kilitendeka ambacho kiliharibu Paradiso. Ahmed, ni kitu gani kilichotendeka?"
"Shetani alikuja na kuharibu kila kitu," Ahmed akasema
"Naam". Hamdi akajibu. "Mungu alimkataza mwanadamu asile tunda lililokuwa katika mti wa kutambua tofauti kati ya mema na mabaya, alipomwambia Adamu:-

**MATUNDA YA KILA MTI WA BUSTANI WAWEZA KULA, WALAKINI MATUNDA YA MTI WA UJUZI WA MEMA NA MABAYA USILE, KWA MAANA SIKU UTAKAPOKULA MATUNDA YA MTI HUO UTAKUFA HAKIKA. (1)**

"Lakini shtani alikuja mfano wa nyoka, akawajaribu Adamu na Hawa. Hawakumtii Mungu lakini walikula lile tunda. Matokeo hayo yalileta uharibifu wa mwanadamu. Tangu dhambi ilipoingia katika maisha ya binadamu, kila mmoja amekuwa mwenye dhambi".

"Ni kweli ya kwamba kila mmoja amekuwa mwenye dhambi?" Ahmed akauliza mwenye mashaka, "Ni vigumu kwangu kuyakubali hayo. Ikiwa ni hivyo, je! ni kwa njia gani kila mmoja amekuwa mwenye dhambi?"

"Mwanadamu alikuwa sawa na tunda alilokula" Hmdi akajibu, "Alikuwa mchanganyiko wa wema na mabaya. Wakati mwingine mtu anaweza kuwa na sifa nzuri kwa kutenda mema, na baadaye angependa kwa kutenda mabaya yasiyoaminika: pengine ni hata kumdanganya na kumwibia jirani yake. Dakika moja mtu aweza kuwa na upendo mwingi na mwenye kujali, na dakika inayofuata yu mwenye kujazwa na wivu, ghadhabu, choyo, na mwenye tamaa au tabia zingine ambazo zinahusiana na dhambi. Kama ulivyosema, Ahmed, kila mwanadamu anashindana na shida hiyo. Kila mashehebu yanashughulika na shida hiyo. Kila taifa linatunga sheria kupunguza dhambi ya aina mbalimbali Kibaya zaidi ni kwamba watu si wenye dhambi kwa sababu wanatenda dhambi. lakini wanatenda dhambi kwa sababu wao ni wenye dhambi. Ni kama kila mtu alivyokuwa na kiwanda kilichotoa dhambi na maovu ndani yake, sivyo?" akauliza Hamdi, huku akamkazia Ahmed macho ya kupenya ndani.

"Ninasikitika kusema kwamba maelezo yako kuhusu mwanadamu yanalingana halisi na hali ya mwanadamu. Kweli watu ni mchanganyiko wa ajabu wa wema na uovu," akajibu Ahmed, "lakini shetani yu ndani ya picha hii kwa njia gani?"

"Basi, ni kwa njia ya dhambi shetani amepata nguvu katika maisha ya wanadamu na katika jumuiya, "akajibu Hamdi." Aliyemjaribu Adamu na Hawa anaendelea vivyo hivyo hata sasa. Anaendelea kuwajaribu watu kusudi waendelee kudumu ndani ya dhambi. Na kwa njia ya dhambi shetani anapata nguvu ndani ya maisha ya watu, kwa sababu dhambi ndiyo inayotutenga na Mungu. Ni kwa sababu ya dhambi ulimwengu u kama ulivyo siku hizi. Mungu aliumba vitu vote vizuri, lakini mwanadamu ameleta maovu mengi ulimwenguni, kwa mfano, kwa njia ya vita na udhalimu, pia kwa njia ya kukosana na kuvunja uhusiano na mambo mengine mengi yanayoleta taabu ambayo inaharibu maisha ya watu".

"Unasema ya kwamba Mungu hakutuumba jinsi tulivyo, na ya kwamba dunia ni jinsi ilivyo kwa sababu ya dhambi ya Adamu?" Ahmed akauliza

"Ni hivyo," Hamdi akajibu, "Dhambi ilimwingia binadamu kupitia Adamu kama maandiko yasemavyo:-

**KWA HIYO, KAMA KWA MTU MMOJA DHAMBI ILIINGIA ULIMWENGUNI, NA KWA DHAMBI HIYO MAOUTI; NA HIVYO MAUTI IKAWAFIKIA WATU WOTE KWA SABABU WOTE WAMEFANYA DHAMBI (2)**

"Matokeo mabaya zaidi yalikuwa mauti; mauti ya kimwili na mauti ya kiroho"
"Mauti ya kimwili na kiroho?" Ahmed akastaajabu huku akimtazama Hamdi "Kifo cha kiroho maana yake nini hasa?"
"Basi, Mungu alimwambia mwanadamu kwamba kama angekula tunda angekufa hakika "Hamdi alianza. "Na kwa kuwa Mungu ni mwenye haki na hutenda kulingana na neno lake, mauti ilikuja kwa mwanadamu. Huku kila mmoja atakufa. Na pia mwanadamu alikufa kiroho alipotenda dhambi". "Jinsi gani?" akauliza Ahmed.
"Ni hivyo, matokeo ya dhambi ni kwamba mwanadamu alifukuzwa kutoka Paradiso," Hadi aliju "Alifukuzwa kutoka mahali alipoishi alipokuwa mtakatifu na mkamilifu mbele ya Mungu. Mwanadamu akalazimishwa kuishi nje ya Paradiso. Mwanadamu alikufa kiroho alipotengea na utukufu wa Mungu kwa ajili ya dhambi zake. Dhambi na maovu humtenga mwanadamu na Mungu wake. Kwa ajili ya dhambi sisi wanadamu hatuishi katika uhusiano wa karibu na Mungu. Kwa sababu Mungu ni mtakatifu, hawezi kuwa na uhusiano na dhambi. Hiyo ndiyo sababu inayotufanya tumhitaji Mwokozi (moyoni) kutuokoa kutoka matokeo yote mabaya ya dhambi. Ahmed, unaamini kwamba dhambi zako zote zimeandikwa mahali fulani?"
Ahmed, huku akionekana akihangaika akasema. "Najua zimeandikwa chini na malaika wawili wanaomfuata kila mtu".
"Mungu anajua kila kitu kuhusu sisi," "Hamdi akasema, "Kila tendo zuri na kila tendo baya, kila wazo, kila neno na kila nia (neya). Mbele ya Mungu kila kitu kimeandikwa chini. Unajua jinsi mizani itakavyopima siku ya hukumu (yom ali-hisabu)?" "La, Mungu tu anajua hayo". Ahmed alijibu kwa sauti ya chini.
"Mungu anakupenda Ahmed. Usisahau kwamba Mwana-kondoo wa Mungu. Yesu, mwana wa Mariamu amezichukua dhambi zote. Msamaha umetolewa kwa dhambi zote". Hamdi akasema kimya.

Ahmed alifikiri kidogo kisha akauliza. "Ikiwa Masihi ni mtu wa maana sana, mbona Adamu na Hawa hawakupata nafasi kusikia habari zake?"
"Unaweza kuamini nikisema ya kuwa walipata habari kuhusu Masihi?"

Hamdi akauliza
"La, sidhani iliwezakana kwa wao kusikia kuhusu yeye". Ahmed akajibu."Mungu anampenda mwanadamu na anataka awe na uhusiano naye". Hamdi akaanza. "Hiyo ndiyo sababu alisema juu ya Masihi tangu mwanzo. Hasa katika mazingira yao, Adamu na Hawa kwa hakika walipata ahadi kuhusu Mkombozi ambaye siku moja angemponda shetani na nguvu zake juu ya mwanadamu. Mungu alisema na shetani, huku Adamu na Hawa wakisikia:-

**NAMI NITAWEKA UADUI KATI YAKO NA HUYO MWANAMKE, NA KATI YA UZAO WAKO NA UZAO WAKE; HUO UTAKUPONDA KICHWA, NA WEWE UTAMPONDA KISIGINO. (3)**

"Katika Biblia nzima wavuloana wanarithi majina ya baba zao-kwa mfano mtoto wa Ibrahimu, mtoto wa Yakobo, na kadhalika- lakini hapa Biblia inatujulisha kuhusu uzao wa mwanamke sio wa mwanaume. Mmoja angalikuja ambaye hakuwa na baba, na kwa hiyo anaitwa mtoto wa mwanamke. Mtoto huyu angeponda nguvu za shetani juu ya mwanadamu, na shetani - mfano wa nyoka angejaribu kumwua mtoto wa mwanamke kwa kuponda kisigino chake. Kwa hakika, hicho ndicho kilichotendeka wakati Yesu, mtoto wa Mariamu alipotoa uhai wake kama fidia kwa dhambi za mwanadamu".
"Kumbe!" Ahmed akasema, "Sidhani ya kwamba Mungu tayari alianza kusema kuhusu Masihi kwa watu wa kwanza duniani. Tena ni wazi ya kwamba kiini cha Biblia ni kuhusu Masihi. Umenipa mengi ya kuyafikiria hadi wakati ujao. Hamdi".

"Al-salamo aleikum"
"Aleikum al-salam".

## MTOTO WA IBRAHIMU

"Ninatafiti sana". Hamdi alisema, "nataka kujua unafikirije juu ya injili (Al-Indjil)"
"Kweli ni kitabu cha ajabu". Ahmed akajibu kwa moyo. "Sijawai kusoma chochote kama hicho". Ni jambo la kuvuta kusoma juu ya ishara za Masihi moja moja. Na mafundisho yake mlimani ni ya kustaajabisha. Ni wazi kwamba yale asemayo ni kweli. Anageuza mawazo anapotuangiza kuwapenda maadui zetu kuwaombea wale wanaotutesa. Na mafundisho yake kuhusu maombi ni mbali kabisa na mafundisho mengine niliyosikia. Lazima nikubali kwamba kitabu hiki kimenigusa ndani sana,

lakini zaidi inaonekana kwamba nimepata maswali mengi sawa na majibu".
"Ni ya kupendeza", Hamdi akasema akitabasamu, "ebu tuanze na swali lako la kwanza !"
"Sawa". Ahmed akakubali. "Kwa nini injili inaanza na uzao wa Ibrahimu kupitia Daudi hadi Masihi?"
Baada ya kufikiri kidogo. Hamdi akauliza, "Unaweza kukumbuka yale tuliyoyazungumzia awali, kwamba Biblia inaunganisha pamoja vitabu vingi, lakini kuna kusudi moja katika kitabu kizima?"
"Ndiyo, nakumbuka," Ahmed akajibu.
"Unakumbuka kusudi lake lilikuwaje?"
"Lilihusika na Masihi", Ahmed akajibu.
"JIbu kwa swali lako linahusiana na kusudi hilo", Hamdi akasema.
"Kukubaliana na unabii, ilipasa Masihi awe mtoto wa Ibrahimu pia". Ahmed alifikiri juu ya yote Hamdi alikuwa amemwambia akasema, "Kile umesema ni cha kuvutia, lakini unaweza kueleza kidogo zaidi kuhusu nabii mbalimbali?"
Baada ya kupumua kwa kitambo kirefu kidogo, Hamdi alianza kwa kusema, "Siku moja, karibu maika elfu nne iliyopita, Mungu alisema na Ibrahimu, aliyejulikana kama rafiki mkuu wa Mungu (khalil Allah). Wakati Ibrahimu alikuwa angali akiitwa Abrahamu, Mungu akampa ahadi ambaye ingekuwa na maana kuu kwa wanadamu wote. Katika vitabu vitano vya Musa, tunasoma:-

**BWANA AKAMWAMBIA ABRAHAMU, TOKA WEWE KATIKA NCHI YAKO, NA JAMAA ZAKO, NA NYUMBA YA BABA YAKO, UENDE MPAKA NCHI NITAKAYOKUONYESHA NAMI NITAKUFANYA WEWE KUWA TAIFA KUBWA, NA KUKUBARIKI, NA KULIKUZA JINA LAKO; NAWE UWE BARAKA; NAMI NITAWABARIKI WAKUBARIKIO, NAYE AKULAANIYE NITAMLAANI; NA KATIKA WEWE JAMAA ZOTE ZA DUNIA WATABARIKIWA. (1)**

"Mungu alimwita mtu ambaye hakuwa na watoto, ingawa alikuwa amekaa miaka mimgi tangu alipooa. akamwahidi nchi. Mungu alikuwa kumfanya awe taifa kuu. Jina lake lingejulikana sana. Hayo yote Mungu aliyatimiza kabisa. Lakini zaidi ya yote, Mungu alimwahidi ya kuwa watu wote duniani walikuwa wabarikiwe kupitia Ibrahimu. Katika ahadi hii imo ahadi ya Masihi. Masihi angekuwa mtoto wa Ibrahimu, na kupitia yeye Mungu angebariki dunia nzima". "Lakini unajuaje kwamba ahadi ilikuwa juu ya Masihi na si mtu mwingine?"
Ahmed alitaka kujua.
"Tunaweza kusema kwamba itajulikana vizuri tunaposoma vitabu vitabu vya Musa," Hamdi akajibu. "Baadaye, Ibrahimu alipata watoto wawili wa kiume:

mmoja na mke wake Sara, ambaye,ambaye aliitwa Isaka na mwingine na mtumishi wa nyumba wa Sara aliyeitwa Hajiri, na mtiti huyo ni Ishmaeli. Ingawa Mungu alimbariki Ishmaeli, Mungu alikuwa amesema wazi kwa Ibrahimu, hata kabla ya kuzaliwa kwake Isaka ya kuwa ahadi kumhusu Masihi ilikuwa kutekelezwa kupitia Isaka, aliposema:-

**MUNGU AKASEMA, 'SIVYO, LAKINI SARA MKEO ATAKUZALIA MWANA WA KIUME, NAWE UTAMWITA JINA LAKE ISAKA. NAMI NITAFANYA AGANO LANGU IMARA KWAKE KUWA AGANO LA MILELE KWA AJILI YA UZAO WAKE BAADA YAKE NA KWA HABARI ZA ISHMAELI NIMEKUSIKIA. NIMEMBARIKI, NITAMZIDISHA, NAMI NITAMWONGEZA SANA SANA. ATAZAA MASEYIDI KUMI NA WAWILI, NITAMFANYA AWE TAIFA KUU. bALI AGANO LANGU NITALIFANYA IMARA KWA ISAKA (2)**

"Ndiyo, Ishmaeli, ambaye Mungu alimbariki, alikuwa baba yetu sisi Waarabu." Ahmed akasema, "lakini sisi Waislamu twajua kwamba Mungu aliwatuma wengi wa mitume na manabii wake kupitia uzao wa Isaka".
Hamdi akaendelea, "Isaka alikuwa na watoto wa kiume wawili, Esau na Yakobo Mungu alionyesha, wakati alijifichua kwa Yakobo, katika ndoto kwamba Masihi aliyeahidiwa angekuja kutoka kwa Yakobo akasema:-

**MIMI NI BWANA, MUNGU WA IBRAHIMU BABA YAKO, NA MUNGU WA ISAKA; NCHI HII UILALAYO NITAKUPA WEWE NA UZAO WAKO. NA UZAO WAKO UTAKUWA KAMA MAVUMBI YA NCHI, NAWE UTAENEA UPANDE WA MAGHARIBI, NA MASHARIKI, NA KASKAZINI, NA KUSINI; NS KSTIKS WEWE, NA KATIKA UZAO WAKO, JAMAA ZOTE ZA DUNIA WATABARIKIWA. (3)**

"Ni jambo la kuangalia ya kuwamba wakati Mungu aliposema na Yakobo, alirudia sehemu nyingi za ahadi yake kwa Ibrahimu. "Ahmed akasema. "Sababu ni ya kwamba ni ahadi ile moja inayopitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine." Hamdi akasema, "lakini jinsi unavyoona, Ahmed, ni kupitia mtoto wa Yakobo Mungu angebariki watu wote ulimwenguni."
"Ndiyo, nimeanza kudhani kwamba Masihi atadhihirishwa tena kuwa jambo kuu katika Biblia," Ahmed akajibu kwa furaha.
"NI kweli," Hamdi akasema. "Miongoni mwa watoto wa Israeli walikuwepo watu wa jamaa nyingi. Swali ni kwamba; Je! Mungu alidhihirisha pia Masihi angalitokea jamii gani? Mungu alimteua Daudi na kufanya agano lake na yeye. Katika nabii nyingi, Mungu anaonyesha kwamba Masihi angetoka ukoo wa Daudi. Nabii Isaya, aliyeishi yapata miaka mia mbili baada ya Daudi. annafananisha ukoo wa Yese na shina la mti lililobaki baada ya mti kukatwa (shina)

Baba ya Daudi aliitwa Yese. Kutoka jamii hiyo angetokea yule 'Roho wa Bwana yu juu yake.' Angeleta haki kwa maskini wa ulimwengu. Angeunda ufalme sawa na paradiso; na kila mmoja ndani ya ufalme huo angemjua bwana. Isaya anasema:-

**BASI LITATOKA CHIPUKIZI KATIKA SINA LA YESE, NA TAWI LITOKALOTOKA KATIKA MIZIZI YAKE LITAZAA MATUNDA, NA ROHO YA BWANA ATAKAA JYY YAKE, ROHO YA HEKIMA NA UFAHAMU, ROHO YA SHURI NA UWEZA, ROHO YA MAARIFA NA KUMCHA BWANA.... BALI KWA HAKI ATAWAHUKUMU MASKINI, NAYE ATAWAONYA WANYENYEKEVU WA DUNIA KWA ADILI; NAYE ATAIPIGA DUNIA KWA FIMBO YA KINYWA CHAKE, NA KWA NA KWA PUMZI YA MIDOMO YAKE ATAWAUA WABAYA...NA ITAKUWA KATIKA SIKU HIYO, SHINA LA YESE, LISIMAMALO KUWA ISHARA KWA KABILA ZA WATU, YEYE NDIYE AMBAYE MATAIFA WATAMTAFUTA; NA MAHALI PAKE PA KUPUMZIKIA PATAKUWA NA UTUKUFU. (4)**

"Ebu, tuone kama nimepata haya vizuri!" Ahmed alisema. "Mungu alifichua kwamba Masihi angalikuwa mtoto wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo na Daudi?" "Kabisa!" Hamdi akajibu akikunjua uso wake kwa furaha, "Na tuakisoma injili tunaona kwamba Masihi alizaliwa kuilingana na unabii. Hiyo ndiyo sababu injili inaanza na ukoo ambao unadhihirisha ya kwamba Masihi ni mtoto wa Ibrahimu na Daudi."

"Tena zaidi, jambo kuu la Biblia limejithibitisha kuwa Yesu, mtoto wa Mariamu". Ahmed akasem. "Lakini, Hamdi, nina hakika unafahamu ya kwamba nina maswali mengine magumu zaidi kuyauliza. Lakini nitayahifadhi hadi wakati ujao".

"Al-salamo aleikum"
"Aleikum al-salam".

## MUNGU NI MMOJA

"Unaona nini?" Ahmed aliuliza, akiinua na kuonyesha vidole vitatu. "Ninaviona vidole vitatu na mkono mmoja. "Ahmed alisema akitabasamu, huku akijua yale Ahmed aliyafikiria.
"Hamdi." Ahmed aliendelea, "Unaamini kwamba Mungu ni mmoja au watatu?" "Labda huwezi kuelewa jinsi ninavyoamini" Hmdi alisema. "Lakini lazima ufahamu kwamba ninamwamini Mungu mmoja wa kweli, Mungu aliyeumba

mbingu na dunia, ajuaye kila kitu na apatikanaye kila mahali. Unajua ya kuwa msingi wa imani yangu ni Biblia, na Neno lake Mungu lafundisha kwamba Mungu ni mmoja. Ukweli huu umeandikwa mara nyingi katika Biblia nzima." "Lakini Mungu hawezi kuwa watatu na mmoja", Ahmed akasisitiza. Tena aliviinua vidole vitatu na kusema, "Moja ongeza moja, na ongeza moja, jibu ni tatu lakini sio moja".

"Wewe u Ahmed wangapi?" Hamdi akauliza. "U mmoja au wawili?"

"Ni mmoja," Ahmed akajibu.

"Mungu amekuumba uwe na mwili na roho," Hamdi akaendelea, "Je! mwili wako ni Ahmed?" "Ndiyo."

"Habari ya roho yako, je?" Hamdi akauliza, "ni Ahmed pia?" "Naam," Ahmed akajibu, huku akifahamu kile Hamdi alitarajia kusema. Hamdi akaendelea. "Kwa sababu gani ingekuwa vigumu kwa Mungu kuwa na hali ya utatu ikiwa alituumba sisi na hali mbili: roho na mwili?"

Baada ya muda punde Hamdi alisema, "Tunaweza kusema kwamba Mungu ni mwunganisho wa watu watatu mfano mmoja. Na tuone moja mara moja mara moja, jibu lake ni nini, Ahmed?"

"Ni moja, "Ahmed akajibu kwa sauti kimya. "Lakini Yesu, mtoto wa Mariamu, ni mwanadamu tu si mtoto wa Mungu". Ahmed alikuwa akimtazama kwa makini mwenzake Hamdi. "Unaamini kwamba Masihi ni Mwana wa Mungu, Hamdi?"

"Unafikiri ninaamini nini?" Hamdi akauliza.

"Sina hakika kamili," Ahmed alisema, "lakini nadhani unaamini kwamba Mungu alikuwa na uhusiano wa kimwili na Bikira Maria na walikuwa na mtoto wa kiume pamoja."

"Ninamwomba Mungu msamaha!" Hadi aksema na nguvu. "Siyaamini haya hata kidogo na simjui mfuasi wa Masihi aliye na imani kama hiyo hata."Ahmed akishangaa, akauliza, "Basi unaamini nini?"

"Naamini Mungu ni wa milele, na alikuwako tangu milele, kabla ya vitu vyo vyote kuumbwa," Hamdi alianza. "Injili inapoeleza Masihi ni nani, haianzi na kuzaliwa kwake katika ulimwengu, lakini inanza na 'Umilele', kabla Mungu hajaumba ulimwengu. Imeandikwa katika Injili:-

**HAPO MWANZO KULIKUWAKO NENO, NANE NENO ALIKUWAKO KWA MUNGU NAYE NENO ALIKUWA MUNGU. HUYO MWANZO ALIKUWAKO KWA MUNGU. VYOTE VILIFANYIKA KWA HUYO; WALA PASIPO YEYE HAKIKUFANYIKA CHO CHOTE KILICHOFANYIKA. NDANI YAKE NDIMO ULIMOKUWA UZIMA, NAO ULE UZIMAULIKUWA NURU YA WATU (1)**

"Mungu aliumba ulimwengu kwa njia ya neno lake, sivyo?"

"Ndivyo, hivyo ilivyo. Mungu alisema, 'Iwe hivyo na ikawa hivyo'", Ahmed alijibu. "Kwa hivyo Mungu aliumba ulimwengu aliumba kupitia neno lake", Hamdi akasema, "na neno hili lililotokana na kushuka kutoka kwa Mungu lilikuwa sehemu ya Mungu na lilijaa nguvu zake Mungu na tabia zake zote. Palikuwamo uzima ndani ya neno lake Mungu, na popote neno hili lilipopatikana, uhai uliumwa katika maumbo yake yote".

"Ndiyo, nimekubaliana nawe, lakini maneno haya, 'na neno lilikuwa Mungu' yana maana gani?" Ahmed akauliza

"Kama ningalitoa ushuhuda kortini, hungeweza kutofautisha maneno yangu na mimi mwenyewe," Hamdi akasema "Maneno yangu yangenisimamia na yangekuwa sehemu yangu. Tunapoketi hapa na kuzungumza, maneno yetu ni sehemu yetu, sawa na kusema kwamba tumebainishwa na maneno yetu. Mungualipoumba ulimwengu, neno alilosema ni moja naye. Hatuwezi kumtenga Mungu na neno lake. Neno hili la milele la Mungu, ambalo li moja naye, na kulingana na tabia zake, lilifunuka wazi katika Yesu, mtoto wa Mariamu, kama ilivyoandikwa;-

**NAYE NENO ALIFANYIKA MWILI, AKAKAA KWETU; NASI TUKAUONA UTUKUFU WAKE, UTUKUFU KAMA WA MWANA PEKEE ATOKAYE KWA BABA; AMEJAA NEEMA NA KWELI. (2)**

"Yale Mungu ameyazungumzia juu yake mwenyewe na tia zake zote, yalifichuliwa katika Masihi. Mungu ni mtakatifu. Wakati watu walipoona jinsi Masihi alivyokuwa mtakatifu. wakaona utukufu wa Mungu ndani yake. Mungu ni pendo. Walipomwona Masihi jinsi alivyowapenda watu, wakaona upendo wa Mungu ndani yake. Mungu ni mwenye enzi yote na anajua yote. Wakati watu walipomwona Masihi akitembea juu ya maji akatuliza mawimbi baharini, kutuliza mawimbi na upepo mkali, kutengeneza mkate, kuwaponya vipofu na kuwafufua wafu, wakaona nguvu na utukufu wa Mungu uliodhihirika ndani yake".

"Lakini inawezekanaje, Mungu apatikanaye kila mahali, asawazishwe na mwanadamu?" Ahmed akasisitiza. "Alisahau mbingu wakati alipokuwa ndani ya Masihi?"

"Ahmed," Hamdi akasema, "kama tungalikuwa nje katika bahari kubwa isiyo na mwisho, na kuingiza kikombe au bilauri na kujijaza na maji, kama tungalichunguza maji yale, tungepata kwamba ni sawa na maji yale ya bahari. Ni sawa na Masihi. Mungu wa milele yuko kila mahali. Pia, anajidhihirisha ndani ya Masihi sawa na tabia zake za nguvu yake. Lakini Mungu hapunguki

kwa sababu anajidhihirisha ndani ya Masihi. Angali yeye ndiye asiye na mwisho".
"Lakini Mungu hawezi kujifunua ndani ya mtu". Ahmed akasema.
"Tunawezaje kumwekea Mungu mipaka?" Hawezi kufanya lo lote?"
"La, anaweza kufanya lo lote." Ahmed akajibu. "Lakini siwezi kuamini kwamba amejifunua katika mwanadamu."
"Ni vizuri tukikubali kwamba hili laweza kuleta shida kwetu sisi, lakini si hivyo kwa Mungu ambaye ana uwezo wa kufanya chochote apendacho". Hamdi akasema.
"Kama ulikuwa bado kufahamu hadithi hii, ungesema nini ikiwa mtu angekuambia kwaba Mungu alijifunua katika kijiti kilichowaka moto, na kama alivyosema na Musa kutoka kijiti kile?"
Ahmed alifikiri kwa muda kidogo huku akifurahi moyoni wakati alipofahamu kwamba haingekuwa vigumu zaidi kwa Mungu kujidhihirisha katika mwanadamu kuliko kijiti.
Hamdi akaendelea, "Ahmed, ebu fikiri kidogo, ni nani aliyeitwa 'Mwana kondoo wa Mungu' na 'Neno la Mungu' na Roho wa Mungu? Hata roho wa Mungu ni mmoja naye Mungu. Tunajua kwamba Roho wa Mungu alimfunika Bikira Mariamu, akashika mimba na akamzaa Masihi, kama malaika Gabrieli alivyomwambia:-

**ROHO MTAKATIFU ATAKUJILIA JUU YAKO, NA NGUVU ZAKE ALIYE JUU ZITAKUFUNIKA KAMA KIVULI; KWA SABABU HIYO HICHO KITAKACHOZALIWA KITAITWA KITAKATIFU, MWANA WA MUNGU. (3)**

"Swali ni kwamba, 'Ni nani huyu aliyekuja ulimwenguni kwa njia hii?'
Ahmed, kama ungalikuwa daktari wakati wa Masihi na ingalikuwa wajibu wakokuandika cheti cha kuzaliwa, ungaliandika nini? Jina lake lingekuwa nani?"
"Labda ningeandika Yesu, mtoto wa Mariamu," Ahmed akasema.
"Na jina la mama yake?"
"Basi, hilo lingalikuwa 'Bikira Mariamu'", Ahmed akajibu.
"Na tena jina la baba yake?" Hamdi akauliza akicheka.
"Hakuwa na baba" Ahmed akajibu, huku akikunjua uso wake zaidi.
"Tungeweza kuacha mstari huo tupu kwa sababu hakuwa na baba wa dunia hii." Hamdi akasema, "au tungejiuliza, Anatoka wapi? Asili yake ni ipi, yeye aitwaye Neno la Mungu na Roho wa Mungu? Yeye aliyeshuka kutoka mbinguni ni nani? Yeye mwenyewe alisema:-

**KWA MAANA CHAKULA CHA MUNGU NI KILE KISHUKACHO KUTOKA MBINGUNI NA KUUPA ULIMWENGU UZIMA... MIMI NDIMI CHAKULA CHA UZIMA; YEYE AJAYE KWANGU HATAONA NJAA KABISA, NAYE ANIAMINIYE HATAONA KIU KAMWE. (4)**

**MIMI NDIMI CHAKULA CHENYE UZIMA KILICHOSHUKA KUTOKA MBINGUNI; MTU AKILA CHAKULA HIKI, ATAISHI MILELE. NA CHAKULA NITAKACHOTOA MIMI NI MWILI WANGU, KWA AJILI YA UZIMA WA ULIMWENGU. (5)**

"Ahmed, Yesu alikuja kusudi autoe mwili wake kama dhabihu kwa wanadamu wote. Yeye alaye chakula cha kawaida anapata uzima wa kimwili, lakini ye yote aulaye mkate ulioshuka kutoka mbinguni hupata uzima wa milele. Amwaminiye Masihi na kumpokea hupata uzima ambao ndani yake huondoa njaa na kiu ya Mungu. Hali hiyo mimi nimepata kujua mwenyewe. Masihi ni sadaka kutoka kwa Mungu kwa wewe, Ahmed."

"Si tayari kwa hayo bado," Ahmed akasema kwa unyenyekevu. "Nina mawazo mengi yanayozuzunguka-zunguka kichwani mwangu. NInafahamu sasa kwamba sikujua hata kidogo jinsi unavyomwamini Mungu. Lakini sasa nimeanza kufahamu pole pole jinsi mnavyomtegemea Mungu wa kweli wa pekee aliyejidhihirisha ndani ya Masihi. Unajua ya kuwa nampenda Masihi kwa moyo wangu wote, lakini nina maswali zaidi ambayo ninahitaji yajibiwe.
Lakini tunaweza kuzungumza juu ya hayo wakati ujao, si hivyo, Hamdi?"
"Natarajia hayo," Hamdi akajibu.

"Al-salamo aleikem"
"Aleikum al-salam",

## MUNGU NA MWANADAMU

"Nimekuwa nikifikiria karibu kila siku na kila usiku mazungumzo yetu yaliyopita," Ahmed alisema. "Kwanza wasema kwamba Yesu, mtoto wa Mariamu ni mwanadamu. Tena wasema kwamba Mungu alijifunua kwake. Ninataka nijue kweli yeye ni nani. Je! si kweli kwamba mmemfanya Masihi kuwa Mwana wa Mungu ijapokuwa yeye si mwingine ila mtoto wa Mariamu tu?"

"Ahmed," Hamdi alianza, "Jibu kwa swali hilo ni ufunguo kwa uzima wa milele pamoja na Mungu hapa leo hii na milele. Ingekuwa makufuru kama tungemfanya mtu awe kama Mungu. Lakini Biblia yatufundisha kwamba

Mungu alijidhihirisha ndani ya mwanadamu, na si kinyume hiyo sote tunakubali kwamba Masihi alizaliwa kama mwanadamu. Kulingana na manabii. yeye ni mwana wa Ibrahimu, mwana wa Daudi na mwana wa Mariamu pia. Lakini katika unabii uliotolewa zamani/kabla ya kuzaliwa kwake Masihi, Mungu "Unasema kwamba mitume na manabii, kabla ya Masihi, Mungu anatufundisha kwamba angekuja kwetu kama Masihi".

"Unasema kwamba mitume na manabii, kabla ya Masihi, walikwisha sema juu ya Mungu mwenyewe kwamba alikuwa kujidhihirisha ndani yake?" Ahmed akauliza akishangaa.

"Jambo kuu la Biblia ni Masihi, kwa hivyo usishangae kuona kwamba Mungu alikuwa tayari amefunua/ukweli juu ya Masihi kwa njia ya manabii," Hamdi akasema.

"Unionyeshe!" Ahmed akaomba kwa upole, "Nimevutwa sana". Hamdi akafikiri kwa muda mfupi kaboa ya kusema, "Wakati Mungu alipoonyesha nabii Mika - karibu miaka 700 kabla ya kuzaliwa kwake Masihi- kwamba Masihi angezaliwa katika mji wa Bethlehemu, pia alifichua kwamba yeye ambaye angezaliwa alikuwako kitambo kabla ya kuzaliwa kwake. Tunasoma:-

**BALI WEWE, BETHLEHEMU EFRATA, ULIYE MDOGO KUWA MIONGONI MWA ELFU ZA YUDA; KUTOKA KWAKO WEWE ATANITOKEA MMOJA ATAKAYEKUWA MTAWALA KATIKA ISRAELI; AMBAYE MATOKEO YAKE YAMEKUWA TANGU ZAMANI ZA KALE, TANGU MILELE. (1)**

"Kweli, Masihi alizaliwa katika mji wa Bethlehemu, kama ilivyoandikwa katika Injili:-

**YUSUFU NAYE ALIONDOKA GALILAYA, TOKA MJI WA NAZARETI, AKAPANDA KWENDA UYAHUDI MPAKA MJI WA DAUDI, UITWAO BETHLEHEMU, KWA KUWA YEYE NI WA MBARI NA JAMAA YA DAUDI; ILI AANDIKWE PAMOJA NA MARIAMU MKEWE, AMBAYE AMEMPOSA, NAYE ANA MIMBA. IKAWA, KATIKA KUKAA HUKO, SIKU ZAKE ZA KUZAA ZIKATIMI; AKAMZAA MWANAWE, KIFUNGUA MIMBA, AKAMVIKA NGUO ZA KITOTO, AKAMLAZA KATIKA HORI YA KULIA NG'OMBE, KWA SABABU HAWAKUPATA NAFASI KATIKA NYUMBA YA WAGENI. (2)**

"Swali ni hili,. 'Ni nani huyu aliyekuwako kabla ya kuzaliwa kwake hapa ulimwenguni?" Tunaona jinsi yeye mwenyewe alivyosema Wayahudi walioghadhibika pale Yerusalemu:-

**IBRAHIMU, BABA YENU, ALISHANGILIA KWA VILE ATAKAVYOIONA SIKU YANGU; NAYE AKAIONA AKAFURAHI. BASI WAYAHUDI WAKAMWAMBIA 'WEWE HUJAPATA BADO MIAKA HAMSINI, NAWE UMEMWONA IBRAHIM?' YESU AKAWAAMBIA, 'AMIN, AMIN, NAWAAMBIA YEYE IBRAHIMU ASIJAKUWAPO, MIMI NIKO'. (3)**

"Twajua ya kuwa Ibrahimu aliishi hapa kama miaka 2000 kabla ya kuzaliwa kwake Masihi".
"Huku Masihi mwenyewe alidai kwamba alikuwako kabla ya kuzaliwa kwake!" Ahmed akasema. "Lakini ni wapi katika unabii tunasoma kwamba Mungu angejidhihirisha katika Masihi?".
"Hayo yameandikwa katika sehemu nyingi". Hamdi akajibu. "Nabii Isaya anazungumza juu ya yule ambaye angetoka sehemu ile ndogo, mahali Yesu, mtoto wa Mariamu, alipokua. Angesimaisha ufalme wa milele, ambao ungepambanuka na 'amani ya Mungu' Yeye mwenyewe, ambaye pia angekuwa mtoto wa Daudi, angetawala katika ufalme huo milele. Nabii anaeleza Masihi ni nani kupitia majina mbalimbali ambayo amepewa:-

**MAANA KWA AJILI YETU MTOTO AMEZALIWA, TUMEPEWA MTOTO MWANAMUME, NA UWEZA WA KIFALME UTAKUWA BEGANI MWAKE; NAYE ATAITWA JINA LAKE, MSHAURI WA AJABU, MUNGU MWENYE NGUVU, BABA WA MILELE, MFALME WA AMANI. MAONGEO YA ENZI YAKE NA AMANI HAYATAKUWA NA MWISHO KAMWE, KATIKA KITI CHA ENZI CHA DAUDI NA UFALME WAKE; KUUTHIBITISHA NA KUUTEGEMEZA KWA HUKUMU NA KWA HAKI, TANGU SASA NA HATA MILELE. (4)**

"Tunajua ya kuwa majina ambayo Mungu humpa mtu yaeleza sifa za yule mtu. Kwa hivyo yeye nani, Ahmed, aliyepewa majina, 'Mshauri mkuu, Mungu wa kweli, Baba aishiye milele, na Mfalme wa amani'?"
"Picha hii ya Masihi, manabii walimtaja kabla ya kuzaliwa kwake katika maandiko yao, imeanza kuonekana kwangu, "Hamdi akasema. "Lakini inasema kweli kwamba Mungu angekuja katika ulimwengu aliouumba mwenyewe?" "Yohana Mbatizaji (Yahya Abn Zakaria) alisema ya kuwa alitumwa na Mungu kuitengeneza njia kwa Masihi/kusudi/watu waongoke na kumwamini Mungu. Wakati watu walipomwuliza - Yohana yeye ni nani na kwa sababu gani Mungu alimtuma, akajibu na maneno ya nabii Isaya, sura 40, mahali imeandikwa:-

**SIKILIZA, NI SAUTI YA MTU ALIAYE, ITENGENEZENI NJIA YA BWANA; NYOSHENI JANGWANI NJIA KUU KWA MUNGU WETU. KILA BONDE LITAINULIWA, NA KILA MLIMA NA KILIMA KITASHUSHWA; PALIPOPOTOKA PATAKUWA PAMENYOKA, NA PALIPOPARUZA PATASAWAZISHWA; NA UTUKUFU WA BWANA UTAFUNULIWA, NA WOTE WENYE MWILI WATAUONA PAMOJA; KWA KUWA KINYWA CHA BWANA KIMENENA HAYA (5)**

"Picha kutoka nabii Isaya inaonyesha wazi kuja kwake mfalme mkuu. Watu wangetengeneza njia kuu mpya kwake nyikani. Lakini huyu mfalme ajaye ni nani, Ahmed?"
"Naam, kulingana na nabii, yeye ni Bwana, Mungu wetu," Ahmed akajibu kwa unyenyekevu.
"Picha inaonekana wazi." Hamdi akaendelea, "tunaposoma zaidi katika ukurasa ule ule mahali ambapo imeandikwa:-

**WEWE UUHUBIRIYE YERUSALEMU HABARI NJEMA, PAZA SAUTI KWA NGUVU; PAZA SAUTI YAKO, USIOGOPE; IAMBIE MIJI YA YUDA, TAZAMENI, MUNGU WETU! TAZAMENI, BWANA MUNGU ATAKUJA KAMA SHUJAA, NA MKONO WAKE NDIO UTAKAOMTAWALIA; TAZAMENI, THAWABU YAKE I PAMOJA NAYE, NA IJARA YAKE I MBELE ZAKE. ATALILISHA KUNDI LAKE KAMA MCHUNGAJI, ATAWAKUSANYA WANAKONDOO MIKONONI MWAKE; NA KUWACHUKUA KIFUANI MWAKE, NAO WANYONYESHAO ATAWAONGOZA POLEPOLE. (6)**

"Kwa kweli, Masihi alikuja kama mchungaji kwa waaminio. Yeye mwenyewe alisema:-

**MIMI NDIMI MCHUNGAJI MWEMA. MCHUNGAJI MWEMA HUUTOA UHAI WAKE KWA AJILI YA KONDOO. (7)**
"Lakini, Ahmed, ni nani ambaye angekuja kama mchungaji kwa kulingana na unabii?"
"Inanibidi nikubali kwamba ni Bwana Mungu mwenyewe kama ionyeshavyo",Ahmed akajibu, huku akitetemeshwa na maneno ya unabii.
Hamdi akaendelea, "Kama unavyofahamu, Ahmed, nabii hizo kuhusu Masihi zilitimilika katika Yesu, mtoto wa Mariamu. Kabla ya kuzaliwa kwake Masihi, malaika Gabrieli limwendea Zekaria, ambaye ndiye angekuwa baba yake Yohana Mbatizaji. Malaika akamwelekeza Zekaria kwamba angempata mtoto wa kiume na kwamba huyu mtoto angepata kazi ya pekee. Malaika Gabrieli akasema:-

**....NANYE ATAONGOZWA ROHO MTAKATIFU HATA TANGU TUMBONI MWA MAMAYE. NA WENGI KATIKA WAISRAELI ATAWAREJEZA KWA BWANA MUNGU WAO. NAYE ATATANGULIA MBELE ZAKE KATIKA ROHO YA ELIYA NA NGUVU ZAKE, ILI KUGEUZA MIOYO YA BABA IWAELEKEE WATOTO, NA KUWATILIA WAASI AKILI ZA WENYE HAKI, NA KUMWEKEA BWANA TAYARI WATU WALIOTENGENEZWA. (8)**

"Ni nani, kufuatana na injili Yohana Mbatizaji, angetangulia mbele yake, Ahmed"?
"Bwana Mungu wao," Ahmed akajibu.
"Wakati ule ule Yohana Mbatizaji alipokuwa amezaliwa," Hamdi akaendelea, "Zekaria alitabiri juu ya mtoto wake mchanga:-

**NAWE, MTOTO, UTAITWA NABII WAKE ALIYE JUU, KWA MAANA UTATANGULIA MBELE ZA USO WA bWANA UMTENGENEZEE NJIA ZAKE; UWAJULISHE WATU WAKE WOKOVU, KATIKA KUSAMEHEWA DHAMBI ZAO. KWA NJIA YA REHEMA ZA MUNGU WETU, AMBAZO KWA HIZO MWANGAZA UTOKAO JUU UMETUFIKIA. (9)**

"Unaona Ahmed, ya kuwa Yohana Mbatizaji, (Yahya Abn Zakaria) mtoto wa Zekaria - kulingana na maneno ya nabii Isaya, malaika Gabrieli, na maneno ya baba yake Zekaria - angemtangulia Bwana, na kwamba yeye aliyekuja ni Mungu mwenyewe?"
"Ndiyo, ninaamini hayo, na ninadhani kwamba haya yote yalidhihirika wazi wakati Masihi alipokuja," Ahmed akijibu kwa fikira.
"Ndiyo, yote kabisa," Hamsi akasema, "Wakati Bikira Mariamu alimzaa Masihi katika Bethlehemu, mji wa Daudi, malaika wa Bwana aliwatokea wachungaji nje ya mji na akawaambia:-

**MSIOGOPE; KWA KUWA MIMI NINAWALETEA HABARI NJEMA YA FURAHA KUU ITAKAYOKUWA KWA WATU WOTE; MAANA LEO KATIKA MJI WA DAUDI AMEZALIWA, KWA AJILI YENU, MWOKOZI, NDIYE KRISTO BWANA. (10)**

"Ukweli kwamba Masihi ndiye Bwana mwenyewe, umethibitishwa mara nyingi katika Injili. Yeye mwenyewe alisema:-

**MIMI NA BABA TU UMOJA. (11)**
"Mimi tayari nimekuwa na upendo mkuu na heshima kwa Yesu, mtoto wa Mariamu," Ahmed akasema. "Lakini sasa, kwa mara ya kwanza, nafikiri ya kuwa ninaweza kuona picha nzima kuhusu Masihi ni nani na ni kwa sababu gani alizaliwa katika ulimwengu. Ninakushukuru kwa vile ambavyo umechukua wakati mwingi na bidii kunielezea haya, Hamdi."

Ahmed, "Hamdi akasema kwa fikira, "Mungu atutoa msamaha kwa kila dhambi na uzima wa milele kwa imani katika Masihi. Na huyo Masihi, ambaye mwenyewe alishinda mauti na kuwafufua wafu husema:-

**MIMI NDIMI HUO UFUFUO, NA UZIMA YEYE ANIAMINIYE MIMI, AJAPOKUFA, ATAKUWA ANAISHI; NAYE KILA AISHIYE NA KUNIAMINI HATAKUFA KABISA HATA MILELE. JE! UNAYASADIKI HAYO? (12)**

"Ahmed, unataka kupokea zawadi ya Mungu kwa imani katika Masihi?"
"Ndiyo, ninasikia kama kwamba anasimama mlangoni mwangu akigonga," Ahmed akasema huku machozi yakitokea machoni mwake, "Sasa ninawezaje kuipokea zawadi ya Mungu?"
"Si vigumu, "Hamdi akajibu, "Mwombe Mungu kwa maneno yako mwenyewe Ungama dhambi zako. Mungu anayajua yote yanayotuhusu. Pokea msamaha kupitia dhabihu ya Masihi kwako wewe. Ombi kwamba Mungu aingie maishani mwako na roho wake na akupe nguvu kumfuata Masihi. Yeye kupitia dhabihu yake ni mpatanishi kati ya Mungu na wewe. Ukimpokea kwa njia hii kwa imani, kama zawadi ya Mungu kwako, mwujiza utafanyika katika maisha yako. Biblia inasema kwamba utakuwa umezaliwa mara ya pili. Upokee maisha mapya kutoka kwa Mungu. Uingie katika uhusiano mpya na Mungu kupitia kwake Masihi. Na Mungu atakuwa Baba yako na wewe utakuwa mwana wake kama maandiko yasemavyo katika injili kuwahusu wote waompokeao Masihi:-

**BALI WOTE WALIOMPOKEA ALIWAPA UWEZO WA KUFANYIKA WATOTO WA MUNGU, NDIO WALE WALIAMINIO JINA LAKE. (13)**

Wakati walipokwisha omba pamoja na kumshukuru Bwana, Hamdi alisema, akiwa mwenye furaha mkuu, "Karibu katika jamii! Sasa kupitia kwa Masihi, sisi tu ndugu katika jamii ya Mungu."
"Ninawezaje kukushukuru wewe?" Ahmed akasema kwa furaha.
"Mshukuru Mungu na ufanye hivyo kila siku!" Hamdi akajibu. "Tafuta ushirika wa wengine ambao humfuata Masihi sawa na wewe. Sasa unaweza kuomba sala ile Masihi aliyowafundisha wanafunzi wake kuomba:-

**BABA YETU ULIYE MBINGUNI, JINA LAKO LITUKUZWE, UFALME WAKO UJE, MAPENZI YAKO YATIMIZWE HAPA DUNIANI KAMA HUKO MBINGUNI; UTUPE LEO RIZIKI YETU, UTUSAMEHE DENI ZETU, KAMA SISI NASI TUWASAMEHEVYO WADENI NA USITUTIE MAJARIBUNI, LAKINI UTUOKOE NA UYULE MWOVU. KWA KUWA UFLME NI WAKO, NA NGUVU NA UTUKUFU, HATA MILELE. AMINA. (14)**

## ORODHA YA VIFUNGO VYA BIBLIA VYATOKEAVYO KITABUNI HIKI:

### MWANAKONDOO WA MUNGU

1) Warumi 6:23
2) Yohana 1:29
3) Ufunuo 3:20

### DHABIHU YA MUNGU

1) 1Timotheo 2:5-6
2) Waebrania 9:22
3) Isaya 53:4-7
4) Zaburi22:14-18
5) Marko 10:45

### DHAMBI

1) Mwanzo 2:16-17
2) Warumi 5:12
3) Mwanzo 3:15

### MTOTO WA IBRAHIMU

1) Mwanzo 12:1-3
2) Mwanzo 17:19-21
3) Mwanzo 28:13-14
4) Isaya 11:1,2,4,10

### MUNGU NI MMOJA

1) Yohana 1:1-4
2) Yohana 1:14
3.) Yohana 6:33,35
5) Yohana 6:51

### MUNGU NA MWANADAMU

1) Mika 5:2
2) Luka 2:4-7
3) Yohana 8:56-58
4) Isaya 9:6-7